



SIKU 16 ZA UANAHARAKATI 2023

MSHIKAMANO! UWEKEZAJI! HATUA THABITI!

MUONGOZO WA SHUGHULI ZA KAMPENI

○ Utangulizi

Katika mwaka wa 2023, tunaanza safari muhimu ya kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati kwa kuungana tukiwa na mshikamano na kutetea uwekezaji katika kuzuia Ukatili dhidi ya Wanawake. Ili kukuza sauti yetu ya pamoja, kiti ya Kuchukua hatua na Utetezi ya mwaka huu inajumuisha Utepe wa Zambarau na Mweupe, Kitita cha Kampeni, Bango la Kampeni, Jarida, Kalenda na Kadi za Kutia hamasa. Jiunge nasi katika kuunga mkono mshikamano, kuchukua hatua thabiti, na kuwekeza kwenye dunia iliyo salama kwa wote.

1. Fahamu vizuri kuhusu Nyaraka za Kampeni

Seti ya kiti hii ina nyenzo kadhaa za kukusaidia na kukuwezesha wakati wa Siku 16 za Harakati za Kuzuia na Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake.

Muhtasari wa Kampeni unatoa uelewa wa kina wa kampeni, unaojumuisha usuli na mantiki kuhusu kampeni na msingi wa malengo yaliyokusudiwa na kampeni.

Mwongozo wa Shughuli ya Kampeni unapendekeza baadhi ya shughuli unazoweza kujihusisha nazo kama watu binafsi, mashirika na jamii.

2. Andaa Majadilano ya Bango la Kampeni

Bango la kampeni linaonyesha nguvu ya mshikamano. Inatusaidia kutafakari juu ya mfungamano na usaidizi wa kifeministi ambao tumepewa katika maisha yetu. Bango linaonyesha ni kwa jinsi gani tunavyoweza kusherehekea na kuheshimu mfungamano huu maalum ambao umetusaidia kustawi. Unaweza kuyaonyesha mabango haya katika maeneo ya umma au uyatumie kuwashirikisha watu wengine katika kutafakari mshikamano wa kifeministi.



Kuna baadhi ya mapendekezo hapo chini ambayo yanaweza kukuongoza unapotafakari kuhusu Bango:

- Shirikisha maarifa yako kuhusu nguvu ya mshikamano iliyoonyeshwa kwenye bango. Mifungamano hii inaweza kukubalika kwa namna gani ndani ya jamii yako?
- Toa ahadi ya kutoa usaidizi kwa wanawake wengine walio kwenye changamoto. Bunga bongo njia zinazoweza kuchukuliwa ili kusherehekea mifungamano na urafiki wa kifeministi.
- Tambua washiriki wa muhimu miongoni mwa watu binafsi na mashirika, unganeni katika utetezi kuhusu uwekezaji kwenye kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.

3. Jihusishe na Kadi ya Kutia Hamasa

Jikite kwenye nukuu za kina kutoka kwa wafeministi wa Kiafrika zilizopo kwenye Kadi ya Kutia Hamasa. Acha maneno haya yaamshe shauku yako ya mshikamano katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.

Zitumie nukuu hizi katika shughuli za shirika lako na za kijamii, eneza ujumbe wa mshikamano wa kifeministi.

4. Kuwa mbunifu kwa kutumia Jarida cha mshikamano.

Jarida la Mshikamano ndio turubai lako wakati wa kutafakari na kufanya ubunifu. Hivi ni vidokezo vya kukuongoza katika tafakari ya kila siku wakati wa kipindi cha siku 16. Unaweza kufanya tafakari ya faragha halikadhalika na tafakari ya pamoja na majadiliano .Tumia ili kuchunguza zaidi:

- Fikiria wakati ulipopata usaidizi wa kifeministi katika maisha yako ambao ulikusaidia na kukuwezesha kutetea ustawi wako.
- Tafakari juu ya undugu na urafiki wa kfeministi ambao umeshuhudia na ungependa kuuheshimu na kusherehekea.
- Fikiria njia za kuwasaidia na kuwekeza katika ustawi wa wanawake unaowafahamu.
- Chagua nukuu yako uipendayo kutoka kwenye kadi ya kutia hamasa na utafakari jinsi inavyoweza kukuhimiza kwenye kuwekeza katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.

5. Jiunge kwenye Mshikamano kwa kuvaa Utepe Mweupe au wa Zambarau.

Umepokea utepe mweupe au zambarau, kulingana na mahali ulipo.Tepe hizi zina pini za kufungia zinazoonyesha maneno "Zuia Ukatili Dhidi ya Wanawake." Unaweza kusambaza tepe hizi ndani ya jamii yako na kuzivaa ili kuonyesha ushiriki wako katika Kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati, Mshikamano! Hatua thabiti! Uwekezaji! Unaweza kuandaa mijadala katika jamii, na kuhimiza majadiliano juu ya umuhimu wa kuwekeza katika programu za Kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake. Wacha utepe uwe kichocheo cha mazungumzo ya mabadiliko halisi.

6. Fuatilia mwongozo wa Shughuli za Vyombo vya Habari ili uwe na wigo mpana katika mitandao na kuunganishwa na wadau mbalimbali.

Mwongozo wa Shughuli za Vyombo vya Habari unajumuisha kiti ya mitandao ya kijamii ambayo unaweza kuitumia katika kushiriki ujumbe wa Siku 16 za Uanaharakati kwenye majukwaa ya mitandao ya kijamii kama vile Facebook, Twitter, Instagram na WhatsApp. Pia ina mapendekezo ya aina mbalimbali ya kwenye vyombo vya habari, kama vile televisheni, radio na magazeti.

7. Shughuli hizi zisikuwekee kikomo. Jisikie huru kuchunguza na kubuni shughuli zinazofaa zaidi katika jamii yako.

Hizo hapo chini ni shughuli nyingine ambazo unaweza kuzifikiria:

Watu Binafsi:

- Jichunguze na utafakari juu ya urafiki wa kifeministi na usaidizi ambao umepata katika maisha yako.
- Tafakari jinsi usaidizi huu ulivyokusaidia katika kuwekeza kwenye ustawi wako.
- Andika mawazo haya kwenye jarida lako
- Sherehekea urafiki wako wa kifeministi kwa kutoa shukrani zako kwa usaidizi huo.
- Jihusishe kwenye urafiki wa kindugu wa kifeministi kwa kuunga mkono mshikamano.

Mashirika:

- Tenga nafasi ambayo washiriki wanaweza kujadiliana kuhusu jinsi ya kujumuisha sauti za waliotengwa.
- Wezesha mjadala wa kutambua makutano mbalimbali katika vuguvugu la ufeministi.
- Jadili mikakati ambayo mashirika yanaweza kuwekeza katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.
- Tambua nyenzo muhimu, kama vile mafunzo, mipango ya afya na bajeti ili kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake
- Sherehekea urafiki wa kifeministi katika shirika lako unapounga mkono mshikamano dhidi ya upinzani unaohatarisha haki za wanawake na kutetea programu na uwekezaji katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.

Jamii

- Andaa sehemu salama kwaajili ya watu binafsi katika jamii yako ili muweze kuzungumza na kusikilizana.
- Anzisha mazungumzo yanayohusu mfumo dume na mienendo isiyo na usawa wa kijinsia.
- Kuza uelewa na ufahamu katika nafasi hii.
- Himiza mshikamano kwa kukubali mifungamano ya kifeministi na kuhamasisha mipango ya utetezi na uwekezaji kwa ajili ya kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.